MZALENDO.

# Serikali ilivyojipanga kuendeleza sekta uvuvi

Na MWANDISHI WETU

SERIKALI imedhamiria kuendeleza sekta ya uvuvi nchini kwa kuhakikisha inanunua zana bora kwa ajili ya wavuvi ili shughuli hizo ziwe endelevu na kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki katika ofisi za wizara hiyo zilizopo Mtumba jijini Dodoma, wakati wa hafla fupi ya kukabidhi injini sita za kupachika katika boti kwa ajili ya vyama sita vya ushirika wa wavuvi.

Alisema nia ya serikali ni kuona mchango wa pato la taifa katika sekta ya uvuvi, unakua kwa kujenga mazingira mazuri ya kuvua rasilimali za uvuvi zilizopo nchini.

Aliongeza kuwa, injini hizo zenye thamani ya sh. milioni 58.7, zilizogaiwa kwa vyama vya Kabwe wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, Mwamgongo wilaya ya Kigoma Vijijini mkoani Kigoma na Msanda Mkuu wilaya ya Mtwara Vijijini mkoani Mtwara.

Vyama vingine ni Kilwa Kivinje wilaya ya Kilwa mkoani Lindi na Igombe Wilaya ya Ilemela pamoja na Chembaya kilichopo Wilaya ya Bushosa mkoani Mwanza, ni sehemu ya fedha iliyoidhinishwa na serikali kwa ajili kuwasaidia wavuvi.

"Mwaka jana na mwaka huu, serikali imetenga sh. milioni 200 ya kununua vifaa na zana mbalimbali za uvuvi kwa ajili ya wavuvi," alisema.

Katika kuhakikisha wavuvi wanaendelea kupata misaada mbalimbali kutoka serikalini, aliwataka wajiunge katika vyama vya ushirika wa wavuvi vinavyotambulika kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa na taifa na kazi zao ziwe zinafanyika kwa kufuata utaratibu unaoeleweka.

Pia, aliwataka wavuvi kuelimisha wenzao kutoendeleza uvuvi haramu kwa kuwa hauna tija yoyote na husababisha madhara kwa mazalia ya samaki na kuharibu shughuli za uvuvi endelevu.

Naye Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alitoa rai kwa wadau wa sekta ya uvuvi nchini kuwa, kazi ya kukabidhi injini hizo za kupachika katika boti liwe chachu ya wao kujipanga vyema kwa kuwa fursa zipo nyingi katika sekta hiyo.

Ulega aliwataka wadau hao kuhakikisha vyama vyao vya ushirika wa wavuvi, vinakuwa imara na vifanye kazi kwa kufuata utaratibu na kuwa, serikali imejipanga kuhakikisha wavuvi wanainuka na kuchangia zaidi katika pato la taifa kupitia sekta ya uvuvi nchini.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, alisema wizara imekuwa ikitoa injini hizo mara kwa mara kwa vyama vya ushirika wa wavuvi ambavyo vimesajiliwa na kutambuliwa kisheria pindi inapopata fedha.

Pia, alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imekuwa ikitumia vigezo mbalimbali kwa vyama vya ushirika vya wavuvi kupata injini za boti, kikiwemo cha ushiriki wao katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi.

Akizungumza kwa niaba ya wabunge kutoka katika majimbo yaliyotoa vyama sita vya ushirika wa wavuvi, Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Dk. Angeline Mabula, alitaka kuwepo kwa elimu zaidi kwa ajili ya kulinda maeneo yenye mazalia ya samaki na kuwepo uvuaji wa samaki wa vipindi.

Alisema kwa sasa wavuvi wameelewa juu ya uvuvi haramu, hivyo ni vyema kulinda na kusimamia maeneo ya mazalia ya samaki ili yasivamiwe na wavuvi na kuharibu uendelevu wa uvuvi katika maeneo yao.



Scanned with CamScanner

paghale, alithibitisha kushi-
kiliwa kwa watuhumiwa hao
juzi jioni.

Alisema maofisa wa polisi

HABARI LEO UK 17.

# * Sababu machinjio Vingunguti kuchelewa kutoa huduma zatajwa

**Na Innara Dossa, TUDARCo**

KUKOSEKANA kwa chumba cha baridi (cold room), kumekwamisha kuanza kwa machinjio ya kisasa ya Vingunguti yaliyokuwa yaanze kazi tangu Julai, mwaka huu.

Mkuu wa Mkoa, Amos Makalla, alijionea hayo wakati wa ziara yake ya kutembelea Jimbo la Ilala.

Machinjio hayo yalikuwa yaanze kazi rasmi Julai mwaka huu lakini bado hayajaanza hata pale Mkuu huyo wa Mkoa alipoongeza muda hadi Agosti Mosi.

Akizungumza baada ya kufanya ziara hiyo, Makalla alisema hajaridhishwa na kutoanza kazi kwa machinjio hayo na kuagiza halmashauri kuanza mchakato wa kumpata mkandarasi wa kutengeneza chumba hicho cha ubaridi.

"Kaimu Mkurugenzi, mpaka ikifika Jumatatu, mpeleke taarifa kwa Katibu Tawala mkandarasi aliyepatikana kuanza kazi hiyo na ili kuharakisha ujenzi nitataka ukamilike nusu ya muda utakaokuwa umepangwa... yaani kama mkandarasi atasema atakamilisha kazi ndani ya miezi mitatu, basi iwe mwezi mmoja na nusu, afanye kazi usiku na mchana, ujenzi huu ukamilike," aliagiza Makalla.

Scanned with CamScanner

UK 7

aji
gea

iji, Jumaa
kupeleka
spitali ya
kuwasaid-
ka katika
a na wale
biji.
lewa na
mu Mkoa
in Mson-
i apeleke
itali hiyo

kuwa wiz-
emuomba
kunusuru
anaohitaji
atika hos-

aduma ya
ya Wilaya
hiyo pesa
a.
hospitali
akipokea
ge, aliele-
inakabili-
huduma
awasaidie
bayo sasa

idia waja-
ngua kwa
hospitali
moja cha

i wa Mpit-
kali kujen-
erahisisha
ou.

## Kwa Ufupi

### Awataka wafugaji kujali mifugo

**Dar es Salaam.** Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amewataka wafugaji kuithamini shughuli hiyo na kuifanya kwa ufanisi ili kuleta tija zaidi katika sekta hiyo.

Alisema wafugaji ndio wanajua siri, faida na hasara za shughuli hiyo, akisema sekta ya mifugo haina mikwara mingi kama biashara nyingine.

Ndaki alieleza hayo juzi, wakati akifunga mkutano wa siku mbili wa wadau wa mifugo uliokuwa ukijadili masuala mbalimbali, ikiwemo namna ya kuipeleka mbele sekta ya mifugo ili kunufaisha wafugaji na Taifa.

"Lazima tuithamini na kuifanya kwa ubora, ili iweze kutupatia tija katika Taifa. Tusipoithamini na kufuga kwa ubora tutaendelea kuimba ... Tanzania ni ya pili kwa mifugo Afrika lakini tija haitaonekana," alisema.



Scanned with CamScanner